1410/206
KISWAHILI
Novemba 2022
Muda: Saa 3

THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

# NATIONAL CERTIFICATE IN SOCIAL DEVELOPMENT

KISWAHILI

**Muda: Saa 3**

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**

*Mtihani huu una sehemu NNE muhimu:*
***insha, ufahamu, matumizi ya lugha na mbinu na vifaa vya kufundishia.***
*Jibu maswali YOTE kwenye kijitabu ulichopewa.*
*Ni muhimu sana ufuate maagizo uliyopewa mwanzo wa kila sehemu.*
***Majibu yote lazima yaandikwe kwa lugha ya Kiswahili.***

easytvet.com

**Kijitabu hiki kina kurasa 6 zilizopigwa chapa.**

**Watahini ni lazima wahakikishe kuwa kurasa zote za karatasi ya mtihani zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.**

© 2022 The Kenya National Examinations Council

## SEHEMU YA KWANZA: INSHA (alama 20)

*Jibu swali **MOJA** kutoka sehemu hii.*

1. (a) Usalama wa nchi umo mikononi mwa wananchi wenyewe. Fafanua.

   (b) Kidole kimoja hakivunji chawa.

   (c) Umeona tangazo la kazi kwenye gazeti la Taifa Leo. Andika barua kuomba kazi hiyo.

   (d) Andika insha inayoanza kwa:

   Ndoto ya Rukia ya kuwa mwalimu ilianza akiwa katika darasa la tano ...

## SEHEMU YA PILI: UFAHAMU (alama 30)

*Jibu maswali **YOTE** katika sehemu hii.*

2. *Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.*

Jasiri alikuwa kifungua mimba katika familia ya Bw. Kombo na Bi. Zawadi. Alikuwa na mnuna wake aliyeitwa Pambo. Waliishi katika kijiji cha Busara kilichopakana na kijiji cha Mwigo. Katika kijiji hiki cha Busara, wakaazi walielewa fika kuwa umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu. Walisherehekea heri yao pamoja, wakahuzunika pamoja palipotokea **shari**. Wanakijiji wa Mwigo waliwaonea wivu; wakawa wanaiga chochote kilichotendwa na wanabusara.

easylvet.com

Familia nyingi katika kijiji cha Busara ziliishi kwa umaskini. Vitu vingi walivionea ndotoni. Si ajabu basi kuwa Jasiri na Pambo hawakupata elimu walioikamia. Mavazi yao yalikuwa yamechanika virakaviraka. Wawili hawa waling'ang'ania blanketi moja walipolala. Licha ya hayo, Bi. Zawadi aliwafunza wanawe umuhimu wa kufanya kazi. Aliwaamsha kila siku ili waandamane naye kwenye kishamba chao kilichokuwa karibu na kijumba chao chenye paa la nyasi na kuta za matope.

Jasiri alibahatika kuhitimu darasa la nane akajivunia cheti cha kiwango cha K.C.P.E. Pambo naye alikomea darasa la tano; si kwa kupenda bali kwa uchochole wa familia yake. Jasiri na Pambo walijitahidi kondeni kuwasaidia wazazi wao kulima mboga. Kumbe wakati huo wote, Jasiri alikuwa na ndoto iliyokuwa **usiku wa giza** kwa wengi.

Rafiki wa karibu sana wa Jasiri, aliyeitwa Ndalo alikuwa na rununu. Alipenda sana kujipumbaza na maajabu ya ulimwengu yaliyoonekana kwenye mitandao ya kijamii. Si michezo ya kuigiza, si muziki, si kandanda; yote yalimburudisha Ndalo. Jasiri alikuwa akinufaika na burudani hii mara kwa mara kwa kuwa walihusiana kwa karibu sana na Ndalo. Alimfuata Ndalo kila uchao.

Ni wazi kuwa kufuata huku kulikuwa ni kule kwa, fuata nyuki ule asali.

Siku moja, Jasiri alimuomba Ndalo kumsaidia kufanya utafiti kuhusu kilimo cha matunda ya matikitimaji. Ndalo aliangua kicheko na kumwambia Jasiri kuwa mambo ya kilimo ni ya wazee. Jasiri alimwambia Ndalo kwamba ndoto yake ilimwelekeza kwenye kilimo ili siku moja aitwe mkulima mashuhuri. Ndalo naye alimsisitizia Jasiri kuwa yeye alikuwa anasoma ili apate kazi ya ofisi mjini. Jasiri hakusita kumwambia mwenzake kuwa utajiri wake ungetokana na ukulima. Ndalo aliridhia hatimaye wakajitosa kwenye utafiti mtandaoni. Habari walizozipata mle zilimfurahisha Jasiri. Alipowaarifu wavyele wake, walijawa na furaha. Kwa matumaini makubwa Bw. Kombo aliandamana na Jasiri hadi afisi za Kaunti zilizokuwa karibu na kijiji chao. Jasiri alipewa nafasi akajieleza kinagaubaga. Basi hatua hiyo ndiyo iliyokuwa mwanzo wa maisha mapya kwa Jasiri na familia yake. Alipata mkopo wa shilingi elfu tano kwa ajili ya mradi huo.

Serikali ya Kaunti ilikuwa imehifadhi mbegu za kila aina ili kuwafaa vijana **walioazimia** kuzama kwenye shughuli za kilimo. Hii ilikuwa njia ya kuwainua vijana. Jasiri alianza shughuli hizo kwa kishindo. Baada ya miezi mitatu, matikitimaji yalikuwa **yamekomaa**. Wanakijiji walishangaa kwani hakuna hata mmoja aliyewahi kufikiria kuwa mimea hiyo ingenawiri kwenye ardhi hiyo.

Hatua hii ya Jasiri iliipiga familia yake jeki isiyomithilika. Pambo alirejea shuleni akasoma hadi kuhitimu kama mwanasheria. Isitoshe, Jasiri aliweza kuwajengea wavyele wake jumba kubwa la kifahari kutokana na hela zilizopatikana kwa ukulima wa matikitimaji. Yeye mwenyewe akawekeza fedha zake katika biashara ya kununua na kuuza hisa. Pia, alianzisha duka kubwa la jumla. Wanakijiji wengi walizama kwenye kilimo hicho. Maisha ya wengi yalibadilika. Wakaazi wa kijiji cha Mwigo waliamua kuiga matendo ya wanabusara. Vijana wa vijiji vyote viwili walimiminika kwa Jasiri kwa mafunzo kuhusiana na kilimo hiki. Watoto wengi sasa walienda shule kutimiza ndoto zao. Wanavijiji hivi viwili waliungana na kujenga zahanati, afya yao ikaimarika.

easytvet.com

Familia ya Bw. Kombo ilijawa na shukrani kwa Jasiri. Ndalo aliporudi kutoka mjini alipokwenda kutafuta ajira, hakuamini macho yake. Jasiri alimkumbusha tu methali isemayo kuwa, mchagua jembe si mkulima.

**MASWALI**

(a) Ipe taarifa uliyoisoma kichwa mwafaka. (alama 2)

(b) Eleza sababu **mbili** za wanamwigo kutamani kuwa kama wanabusara. (alama 2)

(c) Fafanua shughuli **mbili** za kijamii zilizoendelezwa na wanakijiji cha Busara. (alama 2)

(d) Familia ya Bw. Kombo ilikuwa na changamoto si haba. Thibitisha ukweli wa kauli hii kwa hoja **tano**. (alama 5)

(e) Eleza sifa **nne** za Jasiri kulingana na kifungu. (alama 4)

(f) Eleza manufaa **mawili** ya rununu kwa mujibu wa taarifa. (alama 4)

(g) Toa sababu **tatu** zinazoonyesha kuwa serikali ya Kaunti inawajibika. (alama 3)

(h) Wanabusara walikuwa wazalendo. Tetea kauli hii kwa hoja **mbili**. (alama 2)

(i) Mwandishi ametumia methali gani kuelezea:

(i) Uhusiano kati ya Jasiri na Ndalo? (alama 1)

(ii) Kuwa kazi ni kazi. (alama 1)

(j) Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumika katika kifungu. (alama 4)

(i) shari - shida

(ii) usiku wa giza - [illegible]

(iii) walioazimia - [illegible]

(iv) yamekomaa - kuwa tayari

easytvet.com

## SEHEMU YA TATU: MATUMIZI YA LUGHA (alama 30)

*Jibu maswali YOTE katika sehemu hii.*

3. (a) Onyesha silabi katika neno hili. (alama 1)

*Kumsaidia.*

(b) Geuza sentensi ifuatayo iwe katika umoja. (alama 2)

*Hawa ndio wavuvi wapendao Kambare.*

(c) Eleza maana **mbili** za sentensi ifuatayo. (alama 2)

*Jairo alimpikia nyanya uji.*



kwm-Sar1-dio

(d) Tunga sentensi ukitumia: (alama 4)

(i) Kumbe!

(ii) __enye.

(e) Kanusha sentensi ifuatayo. (alama 1)

*Wagonjwa wakifuata maagizo ya daktari watapata nafuu haraka.*

(f) Akifisha sentensi ifuatayo. (alama 2)

*Chukueni fagio mkafagie zizi la ng'ombe Saida aliwaamuru wanawe.*

(g) Unganisha sentensi zifuatazo kwa kiunganishi mwafaka. (alama 1)

*Daudi alicheza vizuri. Daudi hakushinda.*

(h) Sahihisha sentensi zifuatazo. (alama 2)

(i) Mito za Afrika Kusini zimefurika.

(ii) Viroboto zimejaa chumbani mwake.

(i) Andika sentensi ifuatayo kwa udogo. (alama 1)

*Mti mrefu umeanguka karibu na barabara.*

easytvet.com

(j) Andika katika kinyume. (alama 2)

*Fadhili alizipanga nguo zake akiwa ameketi.*

(k) Taja aina za viwakilishi vilivyotumika katika sentensi ifuatayo. (alama 2)

*Wale wakarimu walituzwa zote.*

(l) Tunga sentensi **mbili** kutofautisha maana za maneno yafuatayo. (alama 4)

(i) zuka

(ii) suka

(m) Tambua tamathali za usemi zilizotumiwa katika sentensi zifuatazo. (alama 2)

(i) Katana ni sungura.

(ii) Mambo yake yameenda mrama.

(n) Taja methali zinazooana na maelezo yafuatayo. (alama 4)

(i) Mafunzo anayopewa mtoto huwa mwongozo wake katika maisha. Azoeshwayo na walezi wake huyashika na ni vigumu kutengana nayo.

Mtoto umleavyo ndivyo akuavyo.

(ii) Jambo linalofanywa bila utaratibu halifaulu.

Haraka haraka haina baraka

## SEHEMU YA NNE: MBINU NA VIFAA VYA KUFUNDISHIA (alama 20)

*Jibu mwaswali yote katika sehemu hii.*

4. (a) Wewe ni kinara wa wanafunzi shuleni mwako. Wanafunzi wengi wanapuuza somo la Kiswahili. Kwa hoja **tano**, waeleze umuhimu wa somo hili. (alama 10)

walimu
mwanafunzi

(b) Kwa hoja **tano**, toa ushauri nasaha kwa vijana wenzako kuhusu jinsi ya kuepuka ugonjwa wa 'Covid-19'. (alama 10)

kuepuka mafuriko
kuosha mikono
kupata chanjo
Barakoa

easytvet.com

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA.**